**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI NZEGA.**

SHULE YA SEKONDARI YA
UFUNDI NZEGA.
S.L.P 256,

TABORA.
TAREHE .........................

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.

....................................

S.L.P ......................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI NZEGA,KIDATO CHA KWANZA 2026.**

1. UTANGULIZI.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya ufundi Nzega (**NZEGA TECHINICAL SECONDARY SCHOOL**),kidato cha Kwanza.Shule hii ni ya seriakali na ni ya bweni kwa kidato cha kwanza hadi cha Nne.Pia ni shule ya mchepuo wa Amali na mchepuo wa jumla,na mchanganyiko wa wasichana na wavulana. Muhula wa masomo unaanza tarehe 13.01.2026 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.01.2026. Muda wa mwisho wa kuripoti shuleni ni saa 10.30 jioni.

Tuna imani kuwa kwa wakati wote utakapo kuwa shuleni utakuwa tayari kupokea ,kujifunza , kutii na kutekeleza maagizo sheria na taratibu zote za shule hii kwa kutumia busara ,hekima, utii na uaminifu mkubwa. Iwapo utakuwa hujaripoti mpaka tarehe **31.01.2026** utakuwa umepoteza nafasi yako. **KARIBU SANA.**

2. **KUHUSU SHULE.**

Shule ya sekondari ya Ufundi Nzega inapatikana kitongoji cha Makomelo, kata ya Ijanija katika Halmashauri ya Nzega Mji mkoani Tabora. Shule ipo umbali wa kilometa **6** toka kituo kipya cha mabasi yaendayo mikoani. Hivyo,shuka kituo kikuu cha mabasi Nzega (STENDI MPYA) tumia usafiri wa bajaji kwa gharama ya **Tsh 5,000.** Mwambie dereva akulete moja kwa moja shuleni.Shule hii imepakana na shule ya Msingi Makomelo.Kwa maelezo zaidi namna ya kufika shuleni wasiliana na namba za simu zilizopo kwenye muongozo huu hapo juu.

Shule hii inafundisha masomo ya mkondo wa Amali (ufundi) na mkondo wa jumla. Mwanafunzi kwa kushirikiana na mzazi au mlezi achague fani moja kati ya fani

CamScanner

zinazotolewa hapa shuleni kwa upande wa ufundi ambazo ni **CARPENTRY & JOINERY WITH METALS** na **PLUMBING &PIPE FITTING.**

SCHOOL MOTTO **Discipline and Hardworking leads to success**

SCHOOL VISION Develop well rounded, confident, responsible and motivated students who aspire to achieve their full potential in the rapidly changing world.

SCHOOL MISSION Provide high quality education that empowers every student with physical, economic and social skills that enables academic potential in this rapidly changing world.

3. VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA.

1. Daftari kubwa kumi kwa ajili ya nukuu (counter book).
2. Daftari ndogo kumi kwa ajili ya mazoezi darasani.
3. Begi rangi nyeusi la mgongoni kwa ajili ya kutunzia na kubebea daftari.
4. Scientific calculator moja.
5. Mathematics set
6. Ruler, karamu za wino ( bluu na nyeusi) na penseli za kutosha.
7. Gloves nzito kwa wanafunzi wa fani za uhandisi.
8. Kamusi ya Kiswahili na Kiingereza.
9. Miwani (safety googles) kwa ajili ya kinga ya macho kwa wanafunzi wa fani ya ufundi.
10. Maski ya vumbi (dust mask) kwa wanafunzi wa fani za ufundi.

4. MALAZI

Shule hii ni ya bweni wanafunzi wote wanatakiwa kulala bwenini, hivyo basi kila mwanafunzi anatakiwa awe na godoro jipya la **sponge ft mbili na nusu la inchi sita.**Shuka mbili rangi ya pinki kwa wasichana na rangi ya bluu kwa wavulana na neti moja ya kuzuia mbu rangi ya bluu bahari.

5. Mambo muhimu ya kuzingatia: -

5.1. <u>SARE YA SHULE WAVULANA.</u>

(a) Sare ya Shule ni Suruali mbili (2) za kitambaa rangi ya **KHAKI** iliyokolea (grade one) zenye linda mbili na pindo chini (turn up) **(suruali chini ziwe na upana wa 17 au 18)**, nyuma iwe na mfuko mmoja, zisiwe za kubana mwili (vimodo) iwe yenye kugusa kiatu na iwe na luksi sita za kuwekea mkanda.

(b) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi.

(c) Viatu ni vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi (flat shoes) jozi mbili.
(d) Soksi jozi mbili nyeusi.
(e) Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi (Mkanda wa begi hauruhusiwi)
(f) Sweta dark blue yenye kola ya V
(g) Ovaroli 01 ya rangi ya DARK BLUE.
(h) T-shirt ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh 15,000.

5.2 <u>SARE YA SHULE WASICHANA</u>

(i) Sare ya Shule ni sketi mbili (2) ndefu rangi ya KHAKI iliyokolea rangi (grade one) inayofunika kifundo cha miguu mshono ya rinda box kubwa mbele na nyuma na pembeni marinda mawili tu.
(j) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi.
(k) Viatu ni vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi (flat shoes) jozi mbili.
(l) Soksi jozi mbili nyeupe.
(m) Sweta dark blue yenye kola ya V
(n) Ovaroli 01 ya rangi ya DARK BLUE.
(o) T-shirt ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh 15,000.
(p) Kwa wasichana wa kiislamu hijabu inatakiwa iwe nyeupe kitambaa cha Haluwa.

SARE ZA KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) MICHEZO NA SAFARI KWENDA NJE YA SHULE.

A. WAVULANA

- Suruali mbili za rangi nyeusi.
- Fulana mbili rangi ya kijivu zenye kola maarufu kama form six zenye Nembo ya shule (Nembo zitawekwa shuleni).
- Track suit moja rangi ya dark blue yenye michilizi meupe kwenye suruali na koti.
- Raba au viatu vya michezo.

B. WASICHANA.

- Gauni mbili za kushindia rangi ya maruni mshono wa solo au mwamvuli, kitambaa cha HALUWA pia gauni lile refu hadi kwenye kiwiko cha mguu.
- Track suit moja rangi ya dark blue yenye michilizi meupe kwenye suruali na koti.
- Raba au viatu vya michezo.
- Khanga doti moja.
- Kwa wasichana wa kiislamu hijabu ya kushindia iwe rangi nyeupe.

**6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

**7. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Makosa ya kitaluma kama vile kutokufanya mitihani, kukwepa vipindi na makosa yanafanana na hayo
3. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/ utoro
4. Kugoma na ama kuhamasisha mgomo
5. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi mwenzake, mwalimu / mlezi na jamii kwa ujumla.
6. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.
7. Kufuga ndevu
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
9. Uvutaji wa sigara
10. Uasherati uhusiano wa jinsia moja au kuoa au kuolewa.
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12. Kusababisha mimba au kupata mimba kwa msichana.
13. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni, vilabu maeneo ya kucheza kamali (playstation) n.k.
14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
15. Kudharau nembo za kitaifa mfano bendera ya Taifa, wimbo wa taifa n.k.

16. Kufanya jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu na kuficha maradhi ya hatari
17. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
18. Kulala nje ya shule bila kibali na kukaa nje ya shule baada ya saa kumi na moja jioni.
19. Kukutwa na silaha bwenini kama vile panga, jembe, kisu, kwanja (vitu vyenye ncha kali)
20. Kuwa nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule.
22. Kugomea adhabu baada ya kukutwa na kosa.
23. Kukaidi maelekezo halali ya viongozi na walimu.

## 8. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

8.1 Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambazo zinajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali

8.2 Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

8.3 Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni, kulipa ada, michango ya maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Nb . Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Aidha shule ina kundi la whatsup la Walimu na wazazi kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali za shule kama taaluma,nidhamu,afya na mengineyo, hivyo kwa mzazi ambaye ana simu yenye whatsaap wasiliana na Mkuu wa Shule na Makamu Mkuu wa Shule ili kuweza kuungwa.

Pia kutakuwa na mkutano wa wazazi wote kwa mwaka wa masomo kadiri ratiba ya shule itakavyoelekeza, taarifa mtaipata kwa njia ya mawasiliano!

Karibu sana katika shule ya ufundi Nzega.

Jina la Mkuu wa shule : MWANAKOMBO JUMA

Mawasiliano ,0767732367; 0714912103

Saini na Mhuri wa Mkuu wa shule ..........................................................

HEAD OF SCHOOL
NZEGA TECHNICAL SCHOOL
BOX 256 NZEGA

NB. *Mwanafunzi harusiwi kuja na nguo za nyumbani kwani atakuwa anashindia sare za shule au za kushindia. Haruhusiwi kuja na simu wala laini ya simu, pia siku ya kuripoti shule mwanafunzi aje akiwa amevaa sare ya truck suit ya dark blue.*

(a) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:**

a) Ndoo mbili ndogo (lita kumi) kwa ajili ya usafi.
b) Sabuni za kutosha kwa ajili ya kufulia na kuogea.
c) Mafuta ya kupaka ya kawaida.(vipodozi na perfume haviruhusiwi)
d) Chombo maalumu chenye mfuniko kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
e) Taulo.
f) Kanda mbili kwa ajili ya kuogea.(siyo yebo) na sendo kwa ajili ya kushindia.
g) Kitambulisho cha shule Tsh5,000.(kitapatikana shuleni)
h) Nembo ya shule tsh 5,000.(kitapatikana shuleni).
i) Sahani (ya bati), kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula.
j) Sanduku la bati (tranka) kwa ajili ya kutunzia vifaa binafsi vya mwanafunzi.
k) Picha 4 (passport size) zipigwe na sare ya shule.
l) Bunda 1 la karatasi (ream A4).
m) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
n) Folder faili moja kwa ajili ya kutunzia taarifa za mwanafunzi.
o) Kila mwanafunzi aje na fagio la chelewa lenye mpini mrefu, panga,kwanja, jembe kwa ajili ya usafi wa nje.
p) Kila mwanafunzi aje na squizer,moper,soft broom na hardbroom kwa ajili ya usafi wa bwenini na vyooni.
q) Kila mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA na kama hana Bima utaunganishwa kwenye bima ya afya ya jamii (CHF) KWA KUCHANGIA Tsh 10,000. Kwa mwaka.
r) Mzazi wa mwanafunzi wa kike anashauriwa kumnunulia mtoto wake taulo za kike (sanitary pads) za kutosha pamoja na nguo za ndani za kutosha.

Note: *Kila mwanafunzi alete sabuni ya maji ni litre 5 kwa ajili ya kusafishia chooni iliyothibitishwa na TBS*

## FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi.................................................................................................Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.......................................................................................................

Nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na nimekubaliana nazo kama mzazi/ mlezi wa mwanafunzi na niko tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

.....................................................

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI NZEGA.

A. FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi.......................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa.......................................................................
3. Mzazi/ Mlezi.......................................................................
4. Uhusiano na Mlezi.......................................................................
5. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi, Mkoa....................................... Wilaya ya....................................Mtaa/Kijiji .................................
6. Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi.......................................................................
7. Kabila............................................. Dini ...................................
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi.......................................................................
9. Wazazi wako hai au wamefariki (weka alama ya √ )

   - Baba (amefariki) ( ) Baba yupo hai ( )
   - Mama (amefariki) ( ) Mama yupo hai ( )

10. Ndugu wengine wa karibu na Mzazi/Mlezi ambao wanaweza kutumika kama walezi wa mwanafunzi kama mzazi/mlezi husika hayupo.

    a. ................................ Mahali ....................No ya simu.................
    b. ................................ Mahali .................... No ya simu................
    c. ................................ Mahali .................... No ya simu................
    d. ................................ Mahali .................... No ya simu................
    e. WhatsApps namba .................................. ( kwa ajili ya taarifa na matokeo)

11. SANDUKU LA POSTA/NAMBA YA WHATUPS LA MZAZI/MLEZI KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO:

    .......................................................................
    .......................................................................
    .......................................................................

MEDICAL EXAMINATION FORM

Medical examination form to completed by government medical officer and return to the Head of school Nzega Techinical secondary school

Student full name........................................................................ ............ age.....................

Blood test examination.........................................................................................................

Stool-test..................................................................................................

T.Btest..........................................................................................................

Asthma......................................................................................................

Eye disorder...............................................................................................

Nose disorder................................................................................................

Eardisorder..........................................................................................

Skindisease..........................................................................................

Anemia......................................................................................................

Chest..........................................................................................................

Operations....................................................................................................

Serious Accidents.........................................................................................

Any other infections disease..........................................................................

Additional information e.g. Physical defects or impairment, chronic or family diseases etc.......................................................................................................................

I certify that I have personally examined Mr./Miss..................................................and found him/her fit unit to purpose studies

Signature.........................................................

Designation.......................................................

(Official rubber stamp) ........................................

Nb. Mwanafunzi ambaye ana matatizo ya kiafya aje na vielelezo kutoka hospitali zinazotambulika na serikali

## B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (Jina la mwanafunzi) ......................................................................................................

Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu zote za shule ya bweni, na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwa shuleni hapa kama mwanafunzi. Nitakapo kiuka kipengele chochote cha shule hivyo adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

................................ ...................

Saini ya Mwanafunzi Mkuu wa Shule